## Maswali

1. Wamisri walipata maji ya kukuza chakula wapi?
2. Ndoto ya Farao ya kwanza ilikuwa nini?
3. Ndoto ya Farao ya pili ilikuwa nini?
4. Nani aliweza kutafsiri maana ya hizo ndoto?
5. Nini ilikuwa maana ya hizo ndoto mbili?
6. Yusufu alimshauri Farao afanye nini?
7. Nani alichaguliwa atawale watu na kukusanya nafaka?
8. Farao alipea Yusufu nini?
9. Yusufu alifanya nini kwa huo mda wa miaka 7 myema?
10. Watu walipata chakula namna gani kwa hiyo miaka saba ya njaa?

## Majibu

1. Wamisri walipata maji kutoka kwa Mto Nile.
2. Farao aliota juu ya n'gombe 7 wembamba waliokula n'gombe 7 wanono lakini hawakunona.
3. Farao aliota juu ya masuke 7 ya nafaka dhaifu yalikula masuke 7 ya nafaka manono .
4. Mungu alionyesha Yusufu maana ya ndoto.
5. Kutakuwa na miaka 7 myema halafu miaka 7 ya njaa.
6. Achagua mtu mwenye hekima aweke chakula wakati wote wa miaka 7 myema.
7. Yusufu alichaguliwa.
8. Pete yake, nguo nzuri, mkufu wa dhahabu na gari la kifalme.
9. Yusufu aliweka nafaka kwa maghala makubwa wakati wa miaka 7 myema.
10. Yusufu aliwapa nafaka kutoka kwa maghala.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 13 Ndoto za Farao

**Kwa Biblia** Mwanzo 41


### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hujua yajayo. Anatujali na anaweza ku-tuokoa kutoka kwa mabaya.

### Somo

Yusufu alikuwa mfungwa Misri. Misri iko mashariki ya kaskazini ya Afrika na ina joto jingi. Kwa sababu hakuna mvua nyingi Misri, Mto wa Nile ni wa maana sana kwa hiyo nchi. Wamisri hutumia maji ya Mto wa Nile_kwa kuguza mimea yao. Nile ni mto bora sana. Kwa urefu ni mto wa tatu ulimwenguni. Mto wa Nile inaanzia Ziwa la Victoria nchini Uganda na ina urefu wa maili 5,600.

Kila wakati wa masika kingo za Mto wa Nile hufurika. Wamisri hutumia maji yaliyofurika kwa kilimo. Kuna wakati hakuna maji kwa milima ya chanzo ya Nile. Inamaanisha hakuna mafuriko kwa hivyo hakuna maji.
Hii inasababisha ukame nchini Misri.



*Hekalu ya Misri kando ya Mto Nile*

Usiku moja Farao alikuwa na ndoto zisizo za kawaida. Aliota kwamba alikuwa anatembea kando ya Mto Nile. Aliona n'gombe saba wanono wakila nyasi uwanjani. Alipokuwa bado anaangalia, n'gombe wengine saba wembamba wenye njaa nao wakatoka kwa mto. Wale n'gombe saba wembamba wakala wale n'gombe saba wanono lakini hawakunona.

Baadaye usiku huo, Farao alikuwa na ndoto zingine. Aliota kwamba aliona masuke saba mema yamejaa. Halafu akaona masuke saba membamba dhaifu yenye yalikuwa yamearibiwa na upepo wa mashariki. Yale masuke membamba yaliyala masuke mema yaliyojaa.



Ilipofika asubuhi Farao alikuwa na wasi wasi juu ya hizo ndoto. Aliita watu wake wenye hekima na kuwauliza maana ya ndoto zake. Hakukuwa hata mmoja aliyeweza kumwambia.

Baadaye mnyweshaji alikumbuka Yusufu aliyemwambia tafsiri ya ndoto yake alipokuwa gerezani. Mnyweshaji aliambia Farao juu ya Yusufu. Yusufu alitolewa gerezani. Alipelekwa kwa Farao.

Yusufu alimwambia Farao kwamba yeye hangeweza kueleza ndoto. Mungu anayejua mambo yote atamwonyesha tafsiri ya ndoto. Yusufu alimwambia Farao kwamba ndoto yake ina maana moja.

Yusufu alimwambia kwamba n'gombe saba wanono na masuke saba mema inaonyesha kutakuwa na miaka saba mizuri. Mavuno yatakuwa mazuri kwa miaka saba katika nchi ya Misri. Kila mtu atakuwa na shibe ya kutosha. N'gombe saba wembamba na masuke saba dhaifu inamaana kwamba baada ya hizo miaka saba ya mavuno mazuri kutakuwa na kiangazi na njaa kubwa. Hakuna mmea utakua na kila mtu atakuwa na njaa.

Yusufu alionya Farao kwamba hakuna budi miaka saba mizuri na miaka saba mbaya itakuweko. Mungu ameonyesha Farao kitakachofanyika. Yusufa alimshauri Farao achague mtu aliye na hekima ili aweke nafaka itakayo kuzwa kwa hiyo miaka saba mizuri. Inapasa kujenga maghala kubwa ya kuweka nafaka nyingi ya hiyo miaka myema. Hiyo itasaidia kuwe na chakula cha kutosha kwa miaka saba ya njaa.

Farao na watu wake wa hekima waliona kwamba huo ulikuwa mpango wa busara. Walichagua Yusufu awe ndiye mtu wa hekima wa kusimamia kuweka nafaka. Farao alichagua Yusufu awe mtawala wa watu. Alimpa pete yake. Akamvalisha nguo safi na kumwekea mkufu wa dhahabu shingoni. Farao alimpa Yusufu gari la kifalme na kumwithinisha kuwa mtawala juu ya watu wa Misri wote. Yusufu alipewa mmoja wa binti wa kuhani kama mkewe. Waliishi kwa nyumba ya kifalme.

Mabadiliko gani kwa maisha ya Yusufu! Yusufu alitolewa kwa gereza na akawa mtu wa mamlaka makuu katika nchi ya Misri –akawa makamo wa Farao. Mungu aliendelea kulinda Yusufu na kutimza kusudi yake.

Wakati wa hizo miaka saba mizuri kulikuwa na vyakula vingi sana. Yusufu alisanya nafaka yote na kujaza maghala makubwa. Kulikuwa na nafaka nyingi isiyohesabika.

Miaka saba ya njaa ikaanza. Hakuna chakula kilichokuzwa nchi nzima ya Misri. Watu walikuwa na njaa na wakamlilia Farao. Yusufu aliwapa watu wa Misri chakula kutoka kwa maghala. Kulikuwa na chakula kingi mpaka Yusufu aliuzia watu wa nchi zingine waliokuwa na njaa pia. Mungu alikuwa amemwonyesha Farao kitakachofanyika. Watu walikuwa na chakula kwa huo mda wa njaa.